East African Journal of Swahili Studies, Volume 6, Issue 1, 2023
Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1395

East African Journal of Swahili Studies
eajss.eanso.org
Volume 6, Issue 1, 2023
Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

Original Article

# Mchango wa Ujumi Mweusi katika Unusura wa Nyimbo za Muziki wa Dansi wa Tanzania: 1970- 2000

*Elihaki Yonazi*[1*]

[1] Chuo Kikuu Kishiriki cha AMUCTA, S.L.P 801, Tabora, Tanzania.
[*] Barua pepe ya mawasiliano : mtengaelihaki@gmail.com
**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1395**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*28 Agosti 2023*

**Istilahi Muhimu**:

*Nyimbo, Ujumi, Ujumi Mweusi, Unusura, Muziki Wa Dansi Wa Tanzania.*

**IKISIRI**

Nyimbo za muziki wa dansi wa Tanzania zilianza nchini Tanzania kipindi cha ukoloni. Nyimbo hizi zinasawiri ujumi mweusi kwa kiasi kikubwa, na zina unusura. Ujumi wa kijamii huwa na dhima muhimu katika kazi za kifasihi za jamii husika. Kila jamii ina ujumi wake. Ujumi wa Waafrika huitwa ujumi mweusi. Huu ni ujumi utokanao na utamaduni wa jamii ya Kiafrika pamoja na mazingira yake. Ujumi huu huweza kutumika kuhakikia kazi za kifasihi za Kiafrika. Makala hii imetumia data za maktabani. Jumla ya nyimbo 8 za kuanzia mwaka 1970-2000 zimetumika. Nyimbo hizo zimeteuliwa kimakusudi, kwa kutumia usampulishaji usonasibu. Uteuzi huo umefanywa kwa zingatia dhima kuu, na ya kipekee, inayojitokeza zaidi kwenye wimbo husika. Mbinu zilizotumika kukusanyia data ni; utazamaji makini, udurusu wa matini na mbinu ya kutalii na kukusanya. Data zimechambuliwa kwa kutumia mkabala wa kitaamuli, na nadharia ya Uhalisia imetumika katika uchambuzi wa data ya utafiti huu. Matokeo ya utafiti wa makala hii yanabainisha kwamba ujumi mweusi una mchango mkubwa katika unusura wa nyimbo teule. Unusura huo umebainika kusababishwa na usawiri, kwa mawanda mapana vipengele mbalimbali vya ujumi mweusi kwenye nyimbo teule. Vipengele hivyo ni; umoja na ushirika, adabu na utii, utu, na matumizi bora ya lugha ya Kiswahili. Hivyo, walengwa wake huvutika kuzisikiliza kwani hugusa mambo yanayojenga ustawi wa jamii yao, hivyo kuwa na unusura. Hivyo, wasanii wanashauriwa kuendelea kutunga nyimbo za muziki wa dansi wa Tanzania zenye usawiri wa ujumi mweusi kwa mawanda mapana. Hali hii itasaidia kuendeleza unusura wa nyimbo hizi, kwa ajii ya usatawi wa jamii ya Watanzania na jamii nyinginezo.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1395

**APA CITATION**

Yonazi, E. (2023). Mchango wa Ujumi Mweusi katika Unusura wa Nyimbo za Muziki wa Dansi wa Tanzania: 1970- 2000 *East African Journal of Swahili Studies*, *6*(1), 289-302. https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1395.

**CHICAGO CITATION**

Yonazi, Elihaki. 2023. " Mchango wa Ujumi Mweusi katika Unusura wa Nyimbo za Muziki wa Dansi wa Tanzania: 1970- 2000". *East African Journal of Swahili Studies* 6 (1), 289-302. https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1395.

**HARVARD CITATION**

Yonazi, E. (2023) "Mchango wa Ujumi Mweusi katika Unusura wa Nyimbo za Muziki wa Dansi wa Tanzania: 1970- 2000", *East African Journal of Swahili Studies*, 6(1), pp. 289-302. doi: 10.37284/jammk.6.1.1395.

**IEEE CITATION**

E., Yonazi, "Mchango wa Ujumi Mweusi katika Unusura wa Nyimbo za Muziki wa Dansi wa Tanzania: 1970- 2000", *EAJSS*, vol. 6, no. 1, pp. 289-302, Aug. 2023.

**MLA CITATION**

Yonazi, Elihaki. " Mchango wa Ujumi Mweusi katika Unusura wa Nyimbo za Muziki wa Dansi wa Tanzania: 1970- 2000". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 6, no. 1, Aug. 2023, pp. 289-302, doi:10.37284/jammk.6.1.1395.

## UTANGULIZI

Nyimbo katika jamii ya mwanadamu zilianza zamani sana. Senkoro (1988) anasema kuwa nyimbo ni mojawapo ya utanzu mkongwe zaidi. Zilianza pale tu mwanadamu alivyopata lugha yake, zikiwa na dhima mbalimbali. King'ei na Kisovi (2005) wanaeleza kuwa kuna aina kuu mbili za nyimbo: nyimbo za asili na zile za kisasa. Nyimbo za asili ni nyimbo za kijamii ambazo zimekuwako tangu kale katika jamii mbalimbali. Nyimbo hizi hazina mmiliki, bali ni mali ya jamii nzima, na mtunzi wake hajulikani. Nyimbo hizi huhusisha bendi ya mtu au kikundi cha watu, ambao huwa ndio wamiliki. Tofauti na nyimbo za asili, mtunzi wa nyimbo za kisasa hujulikana na hujitangaza. Nyimbo za aina hii hurekodiwa, husambazwa, huuzwa kwa faida na huimbwa mahali popote, pawe na tukio la kijamii au bila kuwapo. Nyimbo za kisasa zipo katika aina mbalimbali kutegemeana na eneo na utamaduni wa jamii. Kwa mfano; *reggae* - Jamaica, *sokous* na sebene -Kongo, na nyimbo za muziki wa dansi wa Tanzania.

Assen (2012), Laswai (2015) na Mahenge (2021) wanaeleza kuwa nyimbo za muziki wa dansi wa Tanzania, kwa upande wake, ni aina ya nyimbo zinazotokana na nyimbo za muziki wa *Sokuos* wa Kikongo. Laswai (khj) anabainisha sifa za nyimbo za muziki wa dansi wa Tanzania kuwa ni kutumia maneno ya lugha ya Kiswahili, upigaji wa ala-muziki unaoanza taratibu kusisitiza ujumbe, na kisha kupigwa kwa mwendo wa haraka. Mapigo haya ya mwendo wa harakaharaka huitwa mchemko. Sifa nyingine ya nyimbo hizi ni kuhusisha bendi, na hupigwa moja kwa moja jukwaani. Muziki huu pia hujulikana kama muziki wa Waswahili, hii ni kwa sababu hutumia lugha ya Kiswahili (Askew, 2002). Nyimbo za muziki wa dansi wa Tanzania zilianza hapa nchini Tanzania miaka ya 1930, kipindi cha utawala wa Waingereza. Bendi zake nyingi zilianzia maeneo ya mwambao, mfano Dar es Salaam na Tanga. Aidha, muziki huu ulianza kupitia vikundi vya askari jeshini ambao walikuwa wanapiga bendi zao katika hafla mbalimbali (Kitime, 2013; Laswai, 2015).

Kazi yoyote ya kisanaa hufungamanishwa na ujumi wa jamii yake. Senyamanza (hana mwaka) anaeleza kwamba ujumi ni tawi la falsafa linaloshughulikia dhana ya uzuri, asili ya uzuri, ubaya, utukufu, ufutuhi, ladha na falsafa ya sanaaa. Mawazo ya mtaalamu huyu yanashabihiana na ya Renatus (2018) anayeeleza kuwa, ujumi ni uumbuji au urembo katika sanaa. Ujumi hutumiwa kueleza uchunguzi na suala la uumbuji na uvutiaji katika sanaa kwa kujiuliza, nini kinavutia watu, na kwa nini? Aidha, Senyamanza (khj) anaelezea suala la ujumi kuwa hutokana na mtazamo wa mtu au jamii, na kwamba, ujumi wa kisanaa hufungamana na vionjo vya mtu na kaida za jamii.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1303

Ponera (2014) anaeleza kuwa ujumi una dhima ya kutathmini na kuhakiki, na kuhoji sababu zipi zimeipa kazi fulani ya kisanaa ubora. Vilevile huhusika na kuhakiki sababu za kazi za kisanaa kuwa na kasoro, na kuelezea umuhimu wa kasoro ya kazi hizo kwa jamii. Ubora au ubaya wa kazi fulani ya kifasihi hupimwa kwa kufuatana na idili za jamii husika na mazingira yake. Ponera (khj) anaeleza kwamba ujumi hujishughulisha na kutathmini uzuri au ubora wa sanaa, kwa upande mwingine ubaya au udhalili wa sanaa hizo. Hii ni kwa sababu uzuri hauwezi kuwepo kama hakuna ubaya.

Luhwago (2011) anaeleza kwamba ujumi hutumika kama kipimo cha ubora au uzuri wa kazi za kisanaa kulingana na jamii husika. Kila jamii ulimwenguni ina ujumi wake unaotofautiana na ujumi wa jamii nyingine, kulingana na utamaduni na mazingira yake. Jamii za Afrika zina ujumi wake mahususi uliokuwapo tangu kale, uliotumika katika kutathmini na kuhakiki fasihi yake. Ujumi huo hufahamika kama ujumi mweusi. Zirimu (1973) anasema ujumi mweusi ni uzuri wote wa kiujumi utokanao na jamii ya Kiafrika pamoja na mazingira yake. Aidha, huhusisha vigezo vitumikavyo kuainisha urembo wa sanaa kutokana na mazingira ya Waafrika. Ujumi huu hutumika kuzichambua kazi za kisanaa za Kiafrika kwa kuzingatia ustaarabu, mila, utamaduni, na mazingira ya Kiafrika. Renatus (2018) anaeleza kuwa ujumi mweusi ni uzuri wote unaopatikana katika mazingira ya jamii za Kiafrika kutokana na utamaduni wao. Kwa upande wao Mihale (2011) na Sanga (2012) wanasema ujumi mweusi ni nadharia au mkabala wa kushughulikia fasihi na sanaa mbalimbali za Kiafrika. Aidha, Wamitila (2003) anaeleza kwamba fasihi ya Afrika ina ujumi wake mahususi unaojidhihirisha katika vipengele vikuu vinne ambavyo ni wahusika, madhari, matumizi ya lugha, na utendaji. Njogu na Wafula (2007) wanakubaliana na Wamitila (khj) kuhusu uwepo wa ujumi mweusi, kwa kueleza kwamba ujumi mweusi ni vigezo vinavyotumika kuainisha urembo wa sanaa kutokana na mazingira ya watu weusi.

Zirimu (1973) anaeleza kwamba ujumi mweusi huchanganua maudhui, mbinu za wahusika, mbinu za uandishi pamoja na lugha. Kwa upande wa lugha hujumuisha maeneo kama vile; misemo, methali, na kinaya. Sanga (2012(a) & 2018), Laswai (2015) na Renatus (2018) wanabainisha vipengele vinavyoonesha ujumi mweusi kuwa ni umoja na ushirika, imani za kidini, utii na adabu, utu, uhalisia, ukizinda, makusudio, ushababi pamoja na lugha.

Bukenya, A. S.,Gachanja, M. na J. Nandwa (1997) wanaeleza kwamba ujumi huweza kutumika kama mkabala wa uhakiki wa kazi za kifasihi, na kuonesha ubora au udhalili wa kazi hizo. Aidha, Njogu na Wafula (whj) wanaeleza kwamba ujumi mweusi hutumika kuzichambua kazi za sanaa za Afrika kwa kuzingatia; ustaarabu, mila, tamaduni, na mazingira ya Kiafrika.

Russel (2012), John (2018) na Sanga (2021) wanasema kuwa ujumi mweusi una dhima kubwa sana kwa jamii za Waafrika. Wanaeleza dhima hizo kuwa ni; kuelezea idili za jamii ya Waafrika na utathmini wa maisha ya kila siku ya Waafrika. Aidha, wanafafanua zaidi kwamba dhima hizi husawiriwa katika kazi za kifasihi za Kiafrika, na kusababisha kazi hizo kuwa kubalifu zaidi. Aidha, Mulokozi (2017) anasema kuwa ujumi katika kazi za kifasihi una dhima za kijamii na zile za kiburudani. Anafafanua kwamba ujumi katika kazi za kifasihi huakisi na kuelezea idili za jamii yake, kwa upande wa pili kuifanya kazi hiyo iwe na uzuri kufuatana na jamii yake, hivyo kugusa hisia za wanajamii.

Renatus (2018) anasema, ujumi mweusi unayo nafasi kubwa katika ukubalifu na uhai wa kazi za kifasihi za Kiafrika. Hii ni kutokana na ujumi huu kusawiri idili za maisha ya Waafrika, ambazo kwa kawaida ni endelevu. Kazi za kifasihi zenye maudhui endelevu hudumu kwa muda mrefu. Hali ya kazi za kifasihi kuweza kupambana na vizingiti mbalimbali vya kiwakati, kwa muda mrefu, huku bado zikiwa zinapendwa na kukubalika hujulikana kama unusura (Jilala, 2016). Ponera (2014) anaeleza sababu zinazoleta unusura kwenye kazi za kifasihi kwamba ni kutokana na msuko wake wa kifani na kimaudhui kulenga na kugusa mambo endelevu. Aidha, Jilala

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1303

(khj) anaeleza kuwa mambo yanayodumu kwa muda mrefu ndiyo yanayoleta unusura katika kazi za kifasihi na kinyume chake.

Ponera na Jilala (whj) wanataja nyimbo za muziki wa dansi wa Tanzania kuwa ni miongoni mwa kazi za kifasihi zenye unusura. Kwa mantiki hiyo, makala haya yalidhamiria kuchunguza mchango wa ujumi mweusi katika unusura wa nyimbo za muziki wa dansi wa Tanzania kuanzia mwaka 1970 hadi miaka ya 2000.

## NADHARIA YA UTAFITI

Uchambuzi wa data za makala hii umeongozwa na Nadharia ya Uhalisia. Uteuzi wa nadharia hii unatokana na uwezo wake wa kuonesha uhusiano kwa kiasi kikubwa wa jamii na kazi za fasihi za jamii yake.

### Nadharia ya Uhalisia

Snow (1968) anaeleza kuwa Nadharia ya Uhalisia iliasisiwa huko Ufaransa mnamo karne ya 19 kwa ajili ya kupinga matamanio ya kilimbwende yaliyokuwa ya kinjonzi zaidi yakilinganishwa na taabu zilizokuwa zikiwakabili watu. Uhalisia huashiria uwezo wa kusawiri au kuelezea hali kwa kuzingatia uyakinifu wa maisha katika jamii. Huonesha uwakilishi wa uhalisi wa mambo na hali ya kijamii vinayodhihirika katika kazi za kifasihi. Huelezea kwamba fasihi inatakiwa kuelezea mambo kwa kuzingatia uyakinifu wa maisha na uwakati (Moore, 1976; Njogu & Wafula, 2007; Badru, 2015).

Miongoni mwa waanzilishi wa Uhalisia ni Gustave Flaubert (1821-1880), Karl Marx (1818-1883), Gyorgy Lucas (1885-1971) na Maxim Gorky (1868-1936). Wamitila (2002) na Wafula, na Njogu (2007), wanaelezea misingi ya nadharia ya Uhalisia kuwa ni;

- Fasihi isawiri na kuelezea mambo kwa kuzingatia uyakinifu wa maisha ya jamii;
- Fasihi iweze kusawiri na kuelezea mabadiliko yanayotokea kwenye jamii yake.
- Fasihi ioneshe utofauti wa usawiri wa uhalisia kutoka jamii moja hadi nyingie, au kutoka mtu mmoja hadi mwingine
- Mitazamo ya kinjozi haina uwezo wa kutatua matatizo ya wanajamii na,
- Fasihi ioneshe matumaini juu ya kizazi cha binadamu. Hili likiashiria kuwa mwanadamu atakuwa mshindi wa matatizo yanayomkabili katika mazingira yake

Nadharia ya Uhalisia ilitusaidia kuonesha uhusiano wa vipengele mbalimbali vya ujumi mweusi, vinavyosawiriwa katika nyimbo teule, na uhalisia wake katika maisha halisi ya jamii ya Watanzania. Aidha, jinsi gani usawiri wa vipengele vya ujumi mweusi, kwenye nyimbo za muziki wa dansi wa Tanzania, na uhalisia wake kwenye maisha ya Watanzania unavyoleta unusura wa nyimbo teule.

## METHODOLOJIA

Makala hii imetumia data za maktabani, ambapo nyimbo 8 za muziki wa dansi wa Tanzania zilizoimbwa kuanzia mwaka 1970 hadi miaka ya 2000, kati ya nyimbo 20 zilizokusanywa zilitumika. Nyimbo hizi zimekusanywa kutoka kwenye CD, *You Tube* na santuri. Usampulishaji usonasibu ulitumika kupata nyimbo 8 zilizotumika katika uchambuzi wa data za makala hii. Nyimbo hizo ziliteuliwa kimakusudi, kwa kuzingatia dhima kuu ya kipekee inayojitokeza zaidi kwenye wimbo husika. Data zilikusanywa kwa njia ya kutalii na kukusanya, utazamaji makini na udurusu wa matini. Nyimbo zilizotumika ni;“*Neema*, *Harusi ya kibena*, *Kisa cha Mpemba*, na *Acha tamaa*. Nyingine ni *Ni majaliwa*, *Mgumba*, *Nimeishi na wazazi wangu* na *Mtaa wa saba”*. Ufafanuzi na uchambuzi wa data za utafiti uliongozwa na mkabala wa kitaamuli.

## MATOKEO YA UTAFITI

Imebainika kwamba sababu kubwa inazozifanya nyimbo za muziki wa dansi wa Tanzania kuwa na

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1303

unusura ni usawiri mkubwa wa ujumi mweusi katika kazi hizo. Aidha, ujumi huu umebainika kuwa na vipengele kuntu vinavyoelezea idili mbalimbali za jamii ya watanzania ambayo ni msingi wa ustawi wa jamii ya Watanzania wa siku hadi siku. Vipengele vya ujumi mweusi vilivyobainika kujitokeza kwa mawanda mapana katika nyimbo teule kutokana na uchunguzi wa mada ya makala hii ni kuelimisha, umoja na ushirika, adabu na utii, imani za kidini, utu; ukarimu na utatuzi wa migogoro. Vingine ni maadili mema, uburudishaji na matumizi ya lugha ya Kiswahili. Vipengele hivi vimejadiliwa kwa kutolewa mifano kutoka katika baadhi ya beti za nyimbo teule, kama ilivyowasilishwa na kujadiliwa hapa chini;

**Kuelimisha**

Kuelimisha ni kipengele mojawapo cha umakusudi. Umakusudio kwa upande wake ni miongoni mwa kipengele cha uzuri wa ujumi mweusi. Kazi za kifasihi katika jamii za Waafrika zilihusishwa na makusudio maalumu ya kijamii. Kuna mambo ambayo yalitakiwa na yale ambayo hayakutakiwa, fasihi ilitumika kama taasisi ya kijamii kuelimisha jamii juu ya mambo yapi yanayofaa na yasiyofaa.

Utafiti huu umebaini kwamba utunzi wa nyimbo za muziki wa dansi wa Tanzania umekidhi kwa kiwango kikubwa umakusudio kwa mujibu wa jamii ya Watanzania katika kuelimisha. Eneo hili kama kipengele muhimu cha ujumi mweusi, lina mchango mkubwa sana katika unusura wa nyimbo teule. Katika kipengele hiki, nyimbo teule zimebainika kusawiri umakusudio wa kuelimisha kupitia maeneo mbalimbali kama vile kuepuka tamaa, uchaguzi wa mke mwema, kuepuka marafiki wabaya, usuluhishi wa migogoro na kuwa na busara. Mifano ya nyimbo zinazojikita katika kuelimisha ni; *Neema*, *Harusi ya Kibena* na *Kisa cha Mpemba*. Kwa mfano, suala la uchaguzi wa mke mwema, kwa mujibu wa idili za Kiafrika, uzuri wa mke huhusisha maeneo matatu; umbo, tabia njema na ucha Mungu (Sanga, 2018). Kupitia nyimbo za *Kisa cha Mpemba*, *Neema* na *Harusi ya Kibena* waimbaji wanaelimisha jamii hususan kwa vijana ambao hawajaoa juu ya aina ya mke mwema. Wanasisitiza suala la tabia njema kama sifa ya mke mwema. Waimbaji wanabainisha kwenye wimbo wa *Neema* ufuatao:

*Wote:* *Neema*

*Ki:* *Mapokezi umeonesha familia*

*Sina la kusema aaaa*

*Amsaidie eeeee uuuu aaaaa*

*Malezi yako yananifanya*

*nizidi kupendeza aaaa*

*Usije ukabadilisha tabia aaa*

*Inayokutawala*

*Uzuri wako unalingana na roho yake*

Chanzo: Mtafiti (2023)

Wimbo huu unaelezea juu ya Neema, kama mke mwenye tabia njema, anayefurahiwa na mumewe na wakwe zake kutokana na tabia zake njema kama vile; ukarimu, upendo na roho nzuri. Hivyo wimbo huu unatekeleza umakusudio wa jamii wa kuelimisha juu ya mke mwema anavyotakiwa awe. Aidha, umetumika kama darasa kwa wanawake wenye tabia mbaya, huelimishwa kuwa kama Neema ili nao wawe wake wema, hivyo kukubalika kwa waume zao na jamii yao kwa ujumla. Nadharia ya Uhalisia inaeleza kuwa kazi za kifasihi hutakiwa kusawiri uyakinifu wa jamii yake, kwa kufanya hivi hukubalika zaidi. Hivyo, suala la tabia njema mfano, kwa mke, ni utamaduni uaosisitizwa miongoni mwa jamii ya watanzania. Hivyo kusawiriwa kwa tabia hizi kwenye nyimbo teule kumechangia kwa kiasi kikubwa kuzifanya kuwa na unusura. Sanga (2018) anasema, kitu huwa kizuri kutokana na sifa ya kukidhi haja ya kazi iliyotarajiwa kiifanye. Anaeleza zaidi kwamba uzuri wa kitu hupatikana wakati kitu kimetimiza makusudio ya kuundwa kwake. Kazi za kifasihi zinazokidhi mahitaji endelevu ya jamii yake

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1303

hupendwa wakati wote. Wamitila (2002) katika kuielezea nadharia ua Uhalisia, anafafanua kwamba upo uyakinifu wa jamii unaosawiriwa na kazi za kifasihi za jamii hiyo kwa kiwango kikubwa. Usawiri wa aina hii ndio unaozifanya kazi husika kupendwa zaidi na kuwa endelevu.

Wimbo mwingine uliobainika kuleta mchango mkubwa katika unusura wa nyimbo teule kupitia kuelimisha ni, *Acha Tamaa*; kama waimbaji wake wanavyobainisha hapa chini:

*Binadamu hukubali afanye mambo*

*ambayo hata si halali juu ya pesa,*

*Yuda alimuuza Bwana Yesu,*

*Kaini alimuua Abel,*

*Vijana wanaopenda sugar mamies*

*ukiwauliza, eti pia wanatafuta,*

*Acha tamaa mwanangu yoh,*

*Amenikanya mama aliyenizaa,*

*Jichunge yeyeh, amesema nami yoyoh*

*Tukitafuta pesa tutaibaa, tabia mbaya,*

*Vijana wanapenda sugar mamy*

*Ukiwauliza eti pia wanatafuta aaaa...*

*Wasichana wanawapenda Sugar dady*

*Ukiwauliza eti pia wanatafuta aaaa*

Chazo: Mtafiti (2023)

Katika dondoo ya wimbo huu waimbaji wananuia kuwaelimisha watu juu ya ubaya wa tamaa mbaya. Wanaeleza kwamba mtu akiwa na tamaa mbaya, hufanya mambo yasiyotakiwa akilenga kupata hela kwa haraka. Wanarejelea kisasili cha Kibiblia, cha Bwana Yesu kuuzwa na Yuda kwa sababu ya tamaa ya hela. Mfano wa wimbo kama huu, hupendwa kusikilizwa tena na tena kama sehemu ya darasa la kufunza jamii mwenendo mwema. Hivyo basi, huwa endelevu, uendelevu huu huchangia pakubwa kuzifanya nyimbo hizi kuwa na unusura. Nadharia ya Uhalisia inasisitiza utunzi wa kazi za kifasihi za Kiafrika kwa kuzingatia uyakinifu wa jamii yake. Miongoni mwa kipengele cha uyakinifu wa jamii ni utamaduni na mazingira ya jamii husika. Kinyume chake, kazi za kifashi zisizo na uyakinifu wa jamii yake hupingwa na watetezi wa nadharia hii. Hali hii huzifanya kazi hizo zisikubalike. Hii ndio maana wimbo huu unakemea tabia mbaya kama vile vijana kuwapenda *sugar mammies*, kwani huu sio ujumi mweusi. Kwa kufanya hivi huuwezesha kukublika, na hivyo kuchangia unusura wa nyimbo hizi.

**Kusisitiza Juu ya Umoja na Ushirikiano**

Umoja na ushirikiano ni idili muhimu katika maisha ya jamii za Watanzania na Afrika kwa ujumla. Renatus (2018) anaeleza kwamba, umoja na ushirikiano ni miongoni mwa kipengele muhimu cha utu, na ujumi mweusi kwa ujumla, tangu kale. Mtaalamu huyu anaeleza zaidi kuwa, jamii za Kiafrika ziliamini kwamba mtu hawezi kuwa mtu bila ya wengine. Hivyo zilisisitiza suala la umoja na ushirikiano katika nyanja mbalimbali za maisha, kama vile shughuli za uzalishaji mali, sherehe, misiba na hata masuala ya burudani. Nyimbo za muziki wa dansi wa Tanzania zimesheheni kipengele kinachosawiri hali hii. Katika jamii za Watanzania na Waafrika kwa ujumla, suala la umoja na ushirikiano ni endelevu. Hata baada ya athari ya mwingiliano na jamii za kigeni, bado kwa kiwango kikubwa umoja na ushirika unaendelezwa miongoni mwa wanajamii. Hivyo, usawiri wa kipengele hiki huchangia kwa kiwango kikubwa kuzifanya nyimbo hizi kuendelea kuwa hai kwa miongo mingi. Kazi za kifasihi zenye kusawiri hali hii hupendwa na kudumishwa, hali hii huzifanya kazi hizi ziwe na unusura. Nadharia ya Uhalisia iliyotumia katika uchanganuzi wa data ya makala hii inaeleza kwamba, jinsi usawiri wa uyakinifu wa jamii kwenye kazi za kifasihi unavyokuwa mkubwa, ndivyo ukubalifu wa kazi husika unanvyoongezeka. Miongoni mwa nyimbo

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1303

zinazosawiri kipengele hiki kwa mawanda mapana ni; *Ni Majaliwa* kama waimbaji wanavyobainisha;

*Wengi wanapokuwa wanaumwa eee,*

*Nani kauona mwaka,*

*kamaliza mwaka,*

*Ni majaliwa yake Mungu*

*kuuona mwaka x2*

*Ni vizuri ndugu kuweka vikao,*

*na kujadili gharama za matibabu,*

*Kuliko kuwatelekeza,*

*bila msaada wowoteeee.*

*Yatupasa kutetea maisha yao,*

*wanapokuwa wanaumwa eeee*

Chanzo: Mtafiti (2023)

Waimbaji wa wimbo huu wanaelezea umuhimu wa umoja na ushirikiano miongoni mwa wanafamilia. Kwamba, ndugu au jamaa wanatakiwa waishi maisha ya umoja, ili mmojawapo anapopatwa na tatizo asaidiwe na wenzake. Ni vigumu mtu kupata msaada kutoka kwa wengine kama hakuna maisha ya ushirika na umoja. Hivyo suala hili ni miongoni mwa vipengele vya uzuri wa ujumi mweusi. Aidha, vipengele hivi vya ujumi wa kijamii huongoza maisha ya kila siku ya jamii husika. Hivyo, umoja na ushirikiano ni kipengele cha ujumi mweusi kinachotambulisha Uafrika. Watu hupenda kuendelea kusikiliza juu ya mambo yanayofungamana na maisha yao ya kila siku, na yenye kuleta ustawi wa jamii yao. Mambo hayo huwa na dhima nyeti miongoni mwa wanajamii hao. Hivyo mtu anapoyasikia mambo hayo kupitia kazi za kifasihi hupenda kuendelea kuyasikiliza tena na tena, kama sehemu ya kujikumbushia na kuyaendeleza. Kwa vijana, nyimbo hizi, zinazosawiri idili hizo za jamii, hutumiwa kama taasisi ya kuwafunza, ili waishi kufuatana na misingi ya jamii yao, na waweze kukubalika.

Hoja kuu ya Nadhari ya Uhalisia hueleza kwamba, kazi za kifasihi hutakiwa kusawiri uhalisia wa ulimwengu wa wanajamii husika. Aidha, kadri kazi hizo zinavyosawiri uhalisia unaofungamana na ujumi wa jamii yake kwa mawanda mapana, ndivyo zinavyokubalika zaidi na kuwa endelevu. Ponera (2014), Jilala (2016) wanasema kuwa unusura wa kazi za kifasihi hutokana na kazi hizo kubeba maudhui endelelevu. Kwa upande wake Renatus (2018) anashadidia hoja hii kwa kusema kuwa, jamii za Waafrika zimejengwa katika utamaduni wa kuishi kijumuiya tangu kale, na kwamba ujumuiya huo ni mojawapo ya msingi mkubwa wa usatawi wa jamii hizo.

Wimbo mwingine unaosawiri umoja na ushirika kwa mawanda mapana, na kuchangia unusura wa nyimbo teule ni; *Mgumba;* Kama waimbaji wake wanavyobainisha hapa chini;

*Wanikumbusha mbali sana eee,*

*Wanikumbusha*

*ugumba wa Rogati Ega wa Katapila*

*Alipolia nilimbembeleza naye akaisikia*

*Sasa nageukia kwako naomba*

*na wewe unisikie eee*

*Eeee mi eeee*

Chanzo: Mtafiti (2023)

Katika dondoo ya wimbo huu waimbaji wanaelezea hali ya ushirikiano aliyopewa mhusika Mgumba baada ya kukumbwa na tatizo la ugumba. Wanaeleza alivyoonewa huruma, na kubembelezwa asilie. Fauka ya hayo, wanaelezea jinsi walivyomsaidia kumwombea kwa Mwenyezi Mungu ili aondokane na tatizo la ugumba. Kimsingi, katika jamii isiyo na umoja na ushirikiano mtu anapopata tatizo

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1303

hushughulika peke yake. Hivyo, umoja na ushirika kama kipengele cha ya ujumi mweusi, kinaposawiriwa kwenye kazi za fasihi huwafanya watu kuvutika ama kwa kuzisikiliza au kwa kuziangalia tena na tena, kama sehemu ya kuwakumbushia umuhimu wa tabia hii miongoni mwao. Kwa vijana hutumika kama darasa juu ya umuhimu wa tabia ya umoja na ushirikiano kwa jamii yao. Hali hii huchangia kwa kiasi kikubwa kuzifanya nyimbo hizi kuwa na unusura.

**Kusisitiza Juu ya Adabu na Utii**

Adabu na utii ni miongoni mwa idili muhimu za Kiafrika. Ustawi na utulivu wa jamii za Waafrika uliaminika kuwapo kwa sababu ya utii na adabu miongoni mwa wanajamii. Faustine, (2017) na Ngatungwa, (2020) waneleza kuwa, kwa Waafrika utii na adabu upo katika darajia; watoto kuwatii na kuonesha adabu kwa wazazi na wakubwa wao, na watu kuwatii na kuwa na adabu na viongozi wao au watu wanaotawala. Mbali na hivyo, kila jamii iliwajibika kuitii miungu/Mungu yake (Mulokozi, 2017). Nadharia ya Uhalisia husisitiza kwamba, kazi za kifasihi za Kiafrika zinatakiwa zitungwe kwa kuzingatia idili za Kiafrika. Kwa kufanya hivi zitakuwa zimesawiri uhalisia wa jamii yake, hivyo kukubalika. Adabu na utii ni kipengele muhimu ambacho hutambulisha idili na ujumi mweusi kwa ujumla katika kazi za fasihi ya Kiafrika. Kwa Waafrika, adabu na utii ni nguzo ya maisha ambayo huwasaidia wanajamii kuepuka migogoro na kuishi maisha ya ustawi na maelewano.

Matokeo ya utafiti wa makala haya yanabainisha kwamba nyimbo za muziki wa dansi wa Tanzania zimesawiri kipengele cha adabu na utii kwa mawanda mapana. Aidha, imebainika kwamba kipengele hiki ni nguzo mojawapo, na muhimu katika unusura wa nyimbo hizi. Hii ni kwa sababu suala hili ni endelevu, kwani jamii hulirithisha kizazi hadi kizazi kama mojawapo ya amali za kijamii. Kimsingi, kila mwanajamii hutakiwa kujifunza utii na adabu ili akubalike kwenye jamii yake. Nyimbo zilizosawiri kipengele hiki kwa wigo mpana ni; *Nimeishi na Wazazi Wangu, Neema, Acha Tamaa, Harusi ya Kibena* na *Kisa cha Mpemba*. Kwa mfano, kwenye wimbo wa *Kisa cha Mpemba*, waimbaji wanaeleza jinsi mhusika, “mke wa mtu” alivyokosa adabu na utii kwa mumewe kwa kuisaliti ndoa yake, na kuwa na mahusiano ya kimapenzi naMpemba. Hali hii inazua mgogoro dhidi ya mumewe, na hatima yake ni mke huyo kupewa talaka na kuachwa.

Aghalabu kila mwanajamii aliyekengeuka kwa kukosa utii na adabu sio tu alitengwa na jamii yake, lakini pia alipatwa na matatizo. Abdulhamid na Baruwa (2006), wanaeleza kwamba watu waliokosa adabu waliepukwa na wanajamii wengine. Hii ilichukuliwa kuwa watu wasiokuwa na adabu ni wabaya, na wenye adabu walichukuliwa kama watu wazuri. Mke wa mtu anayeelezewa katika wimbo huu, aliyerubuniwa na Mpemba, amechukuliwa kama mtu mbaya, na hatma yake ni kuepukwa na kutengwa na wanajamii. Waimbaji wanabainisha kupitia ubeti huu;

> *Tabia ya mke huyu ilianza tangu kitambo*
>
> *Mume alivumilia na kula mapochopocho,*
>
> *kwa shingo upande*
>
> *Oyoooo! Maskini*
>
> *Ndipo siku hiyo baba kamwaga manyanga chini,*
>
> *na kumtafuta Mpemba*
>
> *Mpemba kakimbia...*
>
> *Upweke huu wa mke ameutaka mwenyewe*
>
> *Nani wa kumlaumu,*
>
> *hakuna wa kumlaumu*
>
> *Ki: Aanalia sana, analia sana*
>
> *Ki: Unyumba hakuna*
>
> Chanzo: Mtafiti (2023)

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1303

Wimbo huu unaonesha madhila aliyoyapata mke huyo, na kwa upande mwingine Mpemba, aliyekuwa na mahusiano ya kimapenzi naye, alikimbia baada ya kufuatwa. Adabu na utii hutakiwa kuoneshwa na kila mwanajamii. Mpemba alikosa adabu kwa kuwa na mahusiano ya kimapenzi na mke wa mtu, hali iliyomsababishia matatizo na mwishowe kukimbia nyumbani kwake. Senyamanza (hana mwaka) anaeleza kuwa ujumi hujumuisha uzuri au ubaya. Ubaya huwa na nia ya kusababisha uzuri. Kwa mfano, kupitia ubaya watu huogopa visa vya ubaya husika, hivyo kugeuka na kufanya uzuri. Hivyo kazi za kifasihi zenye kusawiri masuala yanazosisitiza idili za kijamii, kama vile utii na adabu, sio tu zinapendwa na kufurahiwa, lakini pia hutumika kama taasisi ya kufunza, hususani vijana ili wawe wanajamii wema na wanaokubalika kwenye jamii yao. Hivyo, hali hii huzifanya nyimbo kama hizi kupendwa, na hivyo kuendelea kuwa hai kwa muda mrefu. Hii ndio sababu mojawapo iliyobainika kuchangia nyimbo za muziki wa dansi wa Tanzania kuwa na unusura.

Wimbo mwingine uliobainika kusawiri utii na adabu kwa mawanda mapana ni *Neema*. Katika wimbo huu waimbaji wanamwelezea mhusika Neema alivyoonesha tabia njema ikiwamo utii na adabu kwa mumewe, na wakwe zake kwa ujumla. Hivyo kuonekana kukubalika na kuzidi kupendwa na mumewe. Waimbaji wanabainisha:

*Wote:* *Neema*

*Ki:* *Mapokezi umeonesha familia*

*Sina la kusema aaaa*

*Amsaidie eeeee uuuu aaaaa*

*Malezi yako yananifanya*

*nizidi kupendeza aaaa*

*Usije ukabadilisha tabia aaa*

*Inayokutawala*

*Uzuri wako unalingana na roho yako*

Chanzo: Mtafiti (2023)

Wimbo huu unamwelezea mhusika Neema aliyekuwa na adabu na utii, hasa kwa mumewe na wakwe zake. Hali hii inamfanya kukubalika na kusifiwa na mumewe kwamba amemheshimisha. Aidha, anamsisitiza kwamba asije kubadilika kitabia. Kimsingi nyimbo zenye maudhui kama haya hupendwa na huchukuliwa kama sehemu ya watu kujifunza au kujikumbushia maadili mema ya jamii yao. Hali hii huchangia nyimbo hizi kuishi kwa muda mrefu huku zikiendelea kupendwa kwa kusikilizwa, kutazamwa na kuhakikiwa. Nadharia ya Uhalisia inasisitiza kwamba kazi za kifasihi hutakiwa kuwa na uyakinifu kwenye jamii yake. Uyakinifu unapokuwa wa kiwango cha juu, huzifanya kazi husika za kifasihi kuwa kubalifu zaidi na endelevu. Hii ndiyo hoja mojawapo ya nyimbo za muziki wa dansi wa Tanzania kuwa na unusura.

**Kusisitiza Juu ya Utu**

Falsafa ya Waafrika huamini kwamba mtu ni watu. Utu ni neno linalotumiwa kuelezea umuhimu wa mtu kumtendea mwingine sawa na ambavyo angependa naye atendewe. Utu huhusiana na mambo kama vile; kujali, upendo, ukarimu, usuluhishi wa migogoro na‘usisi’ badala ya ‘umimi’ (Mbiti, 2011a). Utu ni sehemu ya maisha ya Waafrika, ni kipengele muhimu cha ujumi mweusi. Kwa Waafrika, kila mwanajamii hutakiwa kuishi kufuatana na utu. Kwa mfano, kuonesha ukarimu, upendo na kujali wengine. Miongoni mwa msingi wa nadharia ya Uhalisia ni, kazi za kifasihi za jamii yake kuendana na uhalisia uliopo kwenye jamii hiyo. Kwa Waafrika‘utu’ni miongoni mwa uyakinifu unaosisitizwa tangu kale, na husawiriwa kwa kiwango cha juu kwenye kazi zao za kifasihi.

Matokeo ya utafiti wa makala haya yanabainisha kwamba nyimbo zote za muziki wa dansi wa Tanzania zinasawiri vipengele vingi vya utu, kama vile; ukarimu, utatuzi wa migogoro, upendo na maadili mema kwa kina. Vipengele hivyo vimebainika kuwa na mchango mkubwa katika

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1303

unusura wa nyimbo za muziki wa dansi wa Tanzania kwa namna mbalimbali, kama inavyoelezwa hapa chini:

***Kusisitiza Juu ya Ukarimu***

Ukarimu ni miongoni mwa kipengele muhimu cha utu. Mtazamo wa Waafrika juu ya kuwakarimu wageni ni kielelezo cha itikadi ya utu. Waafrika huchukulia mgeni kama ni baraka. Mgeni huweza kuja bila taarifa, akapokelewa na kupewa huduma nzuri. Aidha, mgeni anapomtembelea mtu, hukarimiwa na kupewa upekee kuwazidi wenyeji wake. Kwa Waafrika ukarimu ni suala linalofungamanishwa na utamaduni wao, na ni suala endelevu.

Matokeo ya utafiti uliozaa makala haya yanabainisha kwamba ukarimu ni kipengele muhimu kinachochangia kwa sehemu kubwa unusura wa nyimbo za muziki wa dansi wa Tanzania. Kwa mfano katika wimbo wa *Nimeishi na Wazazi Wangu*, waimbaji wanaelezea ukarimu kama tabia njema na muhimu inayorithishwa na kuendelezwa miongoni mwa wanajamii. Waimbaji wanabainisha:

*Huku niliko wazazi wangu sina ndugu*

*Lakini kutokana na wasia wenu wazazi wangu*

*Najiona kama nipo nyumbani*

*Najiona kama niko nyumbani*

Chanzo: Mtafiti (2023)

Katika ubeti wa wimbo huu waimbaji wanamwelezea kijana aliyelelewa vizuri na wazazi wake na kufunzwa tabia njema, ikiwamo ukarimu. Wanaeleza kuwa baada ya kijana huyo kuwa mtu mzima, wazazi wake walimpa wasia juu ya kuwa na utu. Hali hii inaonesha kwamba ukarimu ni miongoni mwa tabia njema na endelevu kwa Watanzania na Afrika kwa ujumla. Aidha, tabia hii hutakiwa kurithishwa kizazi hadi kizazi. Miongoni mwa mbinu ya kumrithisha mtu kitu ni kumfunza na kumpa wasia. Huu ndio msingi wa waimbaji wa wimbo huu kusema “Lakini kutokana na wasia wa wazazi wangu, najiona kama nipo nyumbani” Mtu anapokwenda ugenini na kusema anajiona kama yuko nyumbani inamaanisha amepata ukarimu mkubwa.

Ukarimu ni miongoni mwa tabia inayosisitizwa na kutakiwa kuendelezwa miongoni mwa Waafrika. Yonazi (2019) anashadidia hoja hii kwa kusema, kwenye jamii ya Waasu, ambao ni jamii mojawapo nchini Tanzania, bibiharusi huimbiwa nyimbo mbalimbali zinazomuasa juu ya kuwa na tabia njema. Mtaalamu huyu anabainisha tabia njema mojawapo inayosisitizwa kuwa ni ukarimu. Anaeleza kwamba bibiharusi huaswa kwamba kama hatakuwa mkarimu nyumbani pake patakimbiwa na watu. Hili linathibitisha kwamba ukarimu ni kipengele muhimu cha uzuri wa ujumi mweusi, na kwamba kinasawiriwa kwenye kazi za kifasihi za jamii ya Watanzania.

Tabia ya ukarimu husisitizwa wakati wote miongoni mwa jamii za Kiafrika, Tanzania ikiwa mojawapo. Aidha, ukarimu huchukuliwa kama miongoni mwa amali muhimu za kijamii, hivyo hurithishwa kizazi hadi kizazi. Hivyo nyimbo zenye kusawiri kwa mawanda mapana ukarimu, hupendwa na huwa endelevu katika jamii yake. Jambo hili limebainika kwamba linachangia kwa kiasi kikubwa kuzifanya nyimbo za muziki wa dansi wa Tanzaniakuwa na unusura.

***Utatuzi wa Migogoro***

Utatuzi wa migogoro ni kipengele kingine cha utu. *Harusi ya Kibena*ni miongoni mwa nyimbo teule zinazosawiri dhima ya kusuluhisha migogoro na hivyo kuzifanya nyimbo hizo kuwa na unusura. Kama waimbaji wanavyoeleza;

*Mnafunga ndoa mambo yenu sawa*

*Bwana awe baba*

*Na bibi awe mama wee*

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1303

*Aweke mambo yawe sawa*

*Mnapogombana muombane radhi*

*Na Mungu naye atawaona yeeee*

Chanzo: Mtafiti (2023)

Katika wimbo huu maneno "mnapogombana muombane radhi" yanaelezea suala la utatuzi wa migogoro kwa njia ya amani. Migogoro kwenye jamii ni suala linalotokea mara kwa mara, na usuluhishi wake hutakiwa kutafanyika wakati wote ili jamii iwe na amani, utulivu na ustawi. Hivyo, utatuzi wa migogoro ni suala endelevu. Kipengele hiki cha utu katika ujumi mweusi kimebainika kuwa na mchango mkubwa katika kuzifanya nyimbo teule ziwe na unusura. Hii ni kwa sababu jamii hupenda kuzisikiliza mara kwa mara nyimbo kama hizi, kwa kuwa zinakidhi idili za jamii yao. Katika wimbo huu waimbaji wanawaasa maharusi kwamba wanapogombana waombane radhi ili waishi kwa amani na kuwa na ustawi, na kupata baraka za Mungu. Kwani palipo na migogoro inaaminika hapana baraka za Mungu. Kuombana radhi ni mbinu muhimu ya kusuluhisha migogoro. Wamitila (2002) anaeleza kuwa Uhalisia kwenye kazi za kifasihi hutarajia kutoa picha, za wahusika, madhari na matukio ambayo yanaoana kwa kiasi kikubwa na uhalisia wa jamii yake. Wimbo ulioelezewa hapo juu umefungamana vema na misingi ya nadharia hii, hivyo kuyapa mwegemo mzuri wa kinadharia matokeo ya uandishi wa makala hii.

**Matumizi ya Lugha ya Kiswahili**

Matokeo ya utafiti wa makala haya yanabainisha kwamba nyimbo za muziki wa dansi wa Tanzania, hasa ule wa kabla ya utandawazi, unatumia lugha sanifu na fasaha ya Kiswahili, inayozingatia maadili ya Kitanzania. Aidha, lugha hiyo imebainika kusawiri utamaduni, mazingira, falsafa, itikadi pamoja na vipengele vingine vinavyofungamana na ujumi mweusi. Kimsingi, lugha ni kipengele muhimu katika kazi za kifasihi, na sehemu muhimu ya utamaduni wa jamii yoyote ile. Jamii inayoandikiwa kazi ya kifasihi kwa kutumia lugha yake, iliyosheheni vionjo mbalimbali vya lugha vinavyosawiri jamii hiyo, hujiona ipo karibu zaidi na kazi hiyo. Hivyo, huvutiwa na kazi hiyo na kuipenda zaidi. Hali hii huchangia kwa kiasi kikubwa kuifanya kazi hiyo kupata mashiko na kudumu. Hii ni tofauti na baadhi ya kazi za kifasihi kama vile riwaya pendwa na ushairi wa Bongo fleva, vinavyotumia lugha isiyo na tafsida, na iliyojaa msamiati wa lugha ya mtaani (Samweli M., Amina, J.S., na Akech, J.K 2013). Hali hii husababisha kazi hizo kupendwa na kundi fulani tu la watu, hususan vijana, hivyo kutoweza kukubalika kwa wote. Nadharia ya Uhalisia inaeleza kuwa kazi za kifasihi hutakiwa kuwa na uyakinifu wa jamii yake. Miongoni mwa uyakinifu wa jamii ni lugha na utamaduni wake. Nadharia hii ilituongoza kubaini matumizi ya lugha ya Kiswahili yaliyo na vionjo mbalimbali vya utamaduni wa jamii ya Watanzania, kama kipengele muhimu cha ujumi mweusi kinachojitokeza kwenye nyimbo teule.

Matokeo ya utafiti wa makala haya yamebaini kwamba matumizi ya lugha ya Kiswahili iliyo sanifu na fasaha, pamoja na kubeba vionjo vingine mbalimbali vinavyosawiri ujumi mweusi, yana mchango mkubwa sana katika kuzifanya nyimbo hizi kupendwa na watu wote, hivyo kuchangia kwa kiasi kikubwa katika unusura wake. Njogu na Wafula (2007) na Badru (2015) katika kuifafanua zaidi nadharia ya Uhalisia, wanasema fasihi ni kioo cha jamii, hivyo hutakiwa kuelezea uhalisia wa jamii yake. Wanaeleza zaidi kwamba jinsi kazi ya kifasihi inavyoelezea uhalisia kwa kiwango cha juu, ndivyo inavyokuwa karibu zaidi na jamii yake. Hivyo kupendwa na kuendelea kusomwa, kusikilizwa au kutazamwa mara kwa mara. Kwa kufanya hivi huchangia kuifanya kazi hiyo kuwa na unusura.

Aidha, matokeo ya utafiti huu vilevile yanabainisha kwamba nyimbo za muziki wa dansi wa Tanzania hutumia misemo, methali na lugha ya ishara vinayorejelea mazingira na utamaduni wa Mtanzania kwa kiwango kikubwa, hali hii huleta ukaribu wa hadhira yake. Lugha ni chombo kinachotumiwa na waandishi wa kazi za kifasihi kuibua hisia za jamii. Kadri mwandishi anavyotumia lugha yenye vionjo

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1303

vilivyo karibu na hadhira yake, ndivyo anavyofanikiwa kuziteka hisia za wanajamii hao, hivyo kuifanya hadhira yake izidi kumakinika na kazi hiyo. Kwa Waafrika, lugha ni kipengele cha kiujumi chenye uzuri wa namna mbalimbali (Renatus, 2018). Lugha ya Kiswahili ni mojawapo ya lugha za Kiafrika.

Baadhi ya nyimbo na mifano yake, zilizotumia mbinu mbalimbali za lugha ya Kiswahili ni kama vile; *Mtaa wa saba***.** Waimbaji wake wametumia taswira kama vile *mapaka*, wakimaanisha ulozi, kama inavyobainishwa katika dondoo hapo chini;

> *Ndoto ndoto za ajabu haziishi tulalapo oooh*
>
> *Darini hakusemikani eti, mipaka hayaishi kulialia*
>
> Chanzo: Mtafiti (2023)

Kwa utamaduni wa Waafrika wanyama kama vile bundi na paka, wanapolia karibu na nyumba usiku, huchukuliwa kama ni ishara ya ulozi. Litokeapo hili huhusishwa na ushirikiana, hivyo watu huenda kwa waganga kupiga ramli au hata kuhama eneo hilo, kama hali hiyo itajirudia mara kwa mara. Katika wimbo huu mhusika aliamua kuhama, kama wanavyobainisha waimbaji wake katika dondoo ifuatayo;

> *Sasa nimehamia mtaa wa saba,*
>
> *toka pale nilipokuwa nikikaa zamani*
>
> *Ile nyumba ilikuwa sio nyumba*
>
> *Ilikuwa na mikosi iiii*
>
> *Korasi: Nimehama, nimehama, kuona balaa limenizidi*
>
> *Na mdomo hauishi ndani ya nyumba yoooo jama*
>
> *Ndoto ndoto za ajabu haziishi tulalapo oooh*
>
> *Darini hakusemikani eti, mapaka hayaishi kulialia*
>
> *Usiku kucha usingizi hauji kabisa*
>
> *Watoto hawaishi kuumwa umwaeeeh jama*
>
> Chanzo : Mtafiti (2023)

Masuala ya ushirikiana, na ishara za ulozi kama vile paka weusi au bundi kulia usiku karibu na nyumba, ni masuala yanayoeleweka kwa jamii za Watanzania. Masuala haya yasawiriwapo katika kazi za kifasihi watu huvutika kusikiliza ili kujua hatma yake, kama sehemu ya kujifunza mbinu za kukabiliana nayo, au kujikumbushia tajiriba kama hizo pengine walizowahi kuzipitia. Matumizi ya lugha ya Kiswahili yenye vionjo vinavyoibua hisi kama hivi kwenye uimbaji wa nyimbo za muziki wa dansi wa Tanzania, imebainika yana mchango mkubwa katika unusuara wa nyimbo hizi.

Nadharia ya Uhalisia inasisitiza kwamba kazi za kifasihi hutakiwa kusawiri uhalisia wa jamii yake, katika maeneo mbalimbali. Lugha ni miongoni mwa eneo hilo, uyakinifu wake, ikiwa ni pamoja na vionjo vyake mbalimbali hutakiwa kujitokeza katika kazi za kifasihi za jamii yake. Nyimbo teule zote zimebainika kuwa na uyakinifu kwa kiasi kikubwa wa jamii ya Watanzania katika maeneo mbalimbali. Aidha, uyakinifu huo unafungamana na ujumi mweusi kupitia vipengele vyake mbalimbali. Hali hii ndiyo inafanya nyimbo hizi kuwa na unusuara.

## HITIMISHO

Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kwamba ujumi mweusi una mchango mkubwa katika unusura wa nyimbo za muziki wa dansi wa Tanzania. Hii ni kwa sababu nyimbo hizi husawiri ujumi mweusi kwa mawanda mapana. Sababu hii huzifanya kupendwa na kuwa na mashiko makubwa kwenye jamii yake, hii ni kwa sababu huelezea idili za jamii yake zinazojenga usatawi na utulivu wa kijamii. Hivyo, nyimbo hizi huchukuliwa kama taasisi ya kijamii inayotumika katika kuweka miongozo mbalimbali ya ustawi na utulivu wa jamii ya Watanzania. Hali hii huzifanya nyimbo hizi kuwa na unusura.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1303

Watunzi wa kazi za fasihi ya Kiswahili, hususan nyimbo wanashauriwa kutunga kazi zenye kusawiri ujumi mweusi kwa kiwango kikubwa, ili ziweze kutumika kama taasisi ya kufunza maadili kwa jamii, na kurithisha amali za kijamii. Aidha, kwa kufanya hivi vilevile watasaidia kazi zao zisikumbwe na mtenguo hivyo kuwa na tija kwa jamii ya Tanzania kwa muda mrefu.

Kwa upande wa serikali na vyombo vyake mbalimbali kama vile Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) vinashauriwa kuendelea kusimamia udumishaji wa maadili mema katika utunzi wa kazi za fasihi ya Kiswahili, ikwemo nyimbo, ili ziweze kuleta tija katika jamii nzima kwa ujumla wake. Aidha, kukataza nyimbo zinazokiuka idili za ki-Tanzania na ujumi mweusi kwa ujumla.

**MAREJELEO**


Abdulhamid, M. & Baruwa, A. (2006). *Methali za Kiswahili: Maana na Matumizi*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers.

Askew, K. (2002). *Performing the Nation: Swahili Music and Cultural Politics in Tanzania* (Vol. 2). University of Chicago Press.

Assen, N.V. (2012). *Resonation Muziki wa Dansi in Dar es Salaam Tanzania*. Tasinifu ya Umahiri (Haijachapishwa). African Language and Culture. Leiden Universitry /Africa Studie Centre.

Badru, Z. A. (2015). *Taswira na Ubainishaji wa Mabadiliko ya Kiujumi katika Vitendawili vyaKiswahili: Mfano wa Vitendawili vya Kiswahili*. Tasinifu ya Shahada ya Uzamivu Chuo Kikuu cha Dodoma (Haijachapishwa)

Bukenya, A., Nandwa, J., & Gachanja, M. (1997). *Oral Literature, a Senior Course*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Faustine, S. (2020). Uafrikanishaji katika Riwaya ya Kiswahili. *Mulika Journal*, *38*(1).

Jilala, H. (2016). *Misingi ya Fasihi Linganishi, Nadharia, Mbinu na Matumizi*. Daud Publishing Company, Dar es Salaam

John, B.N. (2018) Uwi ni Sifa ya Ujumi wa Kiafrika? Mifano kutoka Diwani ya Mnyampala, Mashairi ya Saadan na Kivuli cha Mvumo. *Mkwawa Journal of Education and Development, 2,* 20-33.

Laswai, A. (2015). *Ujumi katika Muziki wa Dansi: Nyimbo Teule za Marijani na Ally Choki*. Tasnifu ya Shahada ya Umahiri Chuo Kikuu cha Dodoma, (Haijachapishwa).

Luhwago J. N. (2013). Ujumi *katika Fasihi Simulizi: Mfano kutoka katika Hadithi za Wahehe*. Shahada ya Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dodoma.

King'ei, K., & C. Kisovi. (2005*). Misingi ya Fasihi Simulizi*. Kenya Literature Bureau, Nairobi

Mahenge, E. (2021). Matumizi ya Mbinu ya Usimulizi katika Kuibua Dhamira ya Ukombozi wa Kisiasa Kusini mwa Afrika: Uchunguzi wa Nyimbo Teule za Muziki wa Dansi nchini Tanzania 1940-1990. *Mulika Journal*, *40*(2).

Mbiti, J.S (2011a). *African Religion and Philosophy*. Kampala: East Africa Education Publishers Ltd

Mihale, K. P. (2011). *Ujumi katika Ushairi wa Mnyampala*. Tasnifu ya Shahada ya Umahiri Chuo Kikuu cha Dodoma, (Haijachapishwa).

Moore, H. T. (1976). *Realism and Naturalism.* London: Donald Pizzer

Mulokozi, M.M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili, Kozi za Fasihi Vyuoni na Sekondari.* Macony Printing, Dar es Salaam.

Ngatungwa, F.J. (2020). *Usawiri wa Falsafa ya Kiafrika katika Semi: Mifano kutoka Vitendawili vya Kiswahili. Chuo Kikuu cha Dodoma Tasinifu ya Umahiri (Haijachapishwa)*

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1303

Ponera, A.S(2014). *Utangulizi wa Nadharia ya Fasihi Linganishi.* Kaarljamer Printing Technology, Dar es Salaam

Renatus, R. (2018). *Ujumi wa Kiafrika Katika Tamthiya ya Kiswahili. Mfano kutoka Kinjekitile na Mashetani.* Tasinifu ya M.A (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dododma. Dodoma

Russell, K. M. (2012). *Introduction to African Art.* Austin, TX: St. Andrew's

Sanga, A. N. (2022). Thamani ya Ujumi wa Kiafrika katika Hadithi Fupi Simulizi za Kiswahili. *Mulika Journal*, *40*(1).

Samwel, M., Amina, J.S., na Akech, J.K. (2013) *Ushairi wa Kiswahili Nadharia, Maendeleo, Mwongozo kwa Walimu wa Kiswahili na Diwani ya MEA.* Dar es Salaam: Mevel Publishers (MVT)

Sanga, A. N. (2012). *Ujumi katika Riwaya Pendwa ya Kiswahili: Mifano kutoka kwa Mohamed Said Abdulla na Arstablius Elvis Musiba*. Tasinifu ya Shahada ya Umahiri Chuo Kikuu chaDodoma, (Haijachapishwa).

Sanga, A.N. (2018). *Mkengeuko wa Ujumi wa Kiafrika Katika Hadithi Fupi Andishi za Kiswahili Kipindi cha Utandawazi : Mifano kutoka Magazeti ya Habari Leo, Nipashe Na Mwananchi*. Phd Thesis (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dododma.

Senkoro, F. E. (1988). *Ushairi: Nadharia na Tahakiki*. Dar es Salaam University Press.

Senyamanza, C. R.(hnm). *Misingi ya Kazi za Kubuni, Nadharia, Mbinu na Mifano ya Kibunilizi.* Dar es Salaam: Karlijamer Print Technology.

Snow, C. P. (1968). *The Realists: Portraits of Eight Novelists.* Macmillan: London.Wafula, R. M., &Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi.* The Jomo Kenyatta Foundation, Nairobi.

Wamitila, K.W(2002). *Fasihi Simulizi.* Muwa Publishers Limited, Nairobi.

Wamitila, K.W. (2003). *Fasihi Simulizi*. Muwa Publishers Limited, Nairobi.

Yonazi, E. (2019). *Usanaa wa Lugha katika Ujenzi wa Dhima za Nyimbo za Harusi za Waasu.* Tasinifu ya M.A Kiswahili (Haijachapishwa), Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Zirimu, P. (1973). *Black Aesthetics: Papers from a Colloquium Held at the University of Nairobi, June 1971*. East African Literature Bureau, Nairobi.